- x. Kanuni hizi zimeandaliwa ili kuhakikisha kwamba Chuo Kikuu kinaendeshwa kwa ufanisi na vizuri, na kwamba wafanyakazi wanatendewa kwa haki na kwa usawa. Ni jitihada ya kueleza vizuri na kwa uwazi msimamo wa Chuo Kikuu ili kwamba hatua ya kinidhamu au marekebisho isiwe kama ya kushtukiza kwa wafanyakazi.
- xi. Kanuni hizi zinafafanua viwango vyta chini vyta mwenendo wa ajira na kueleza madhara ya kuzikiuka. Pia, kanuni zinaleza haki za wafanyakazi.
- xii. Kutofuatwa kwa kanuni hizi za maadili au sehemu yake yoyote na mfanyakazi ye yoyote kutakuwa ni kukiuka kanuni ya maadili chini ya sheria ya ajira/mkataba na kutafuatiwa na adhabu inayoruhusiwa.
- xiii. Kanuni hizi za maadili, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo humu au mahali pengine palipolezwa au vinginevyo muktadha utakavyohitaji, zitatumika kwa wafanyakazi wote wa Chuo Kikuu.

-
- xiv. Baraza la Chuo Kikuu linaweza kurekebisha, kuongeza au kubatilisha kanuni au sehemu yake yoyote bila ya kutoa sababu. Usimamizi wa kila siku wa kanuni hizi na jukumu la ufanuzi litakuwa la Menejimenti ya Chuo Kikuu.
 - xv. Pale ambapo sehemu yoyote au kifungu cha kanuni hizi kina mgongano/kinakinzana na Sheria yoyote iliyotungwa au kanuni za Serikali au sheria na Miongozo ya Kanisa, masharti ya sheria hizo au kanuni au miongozo itatumika.
 - xvi. Tarehe ya kuanza kutumika kwa Kanuni ni kuanzia siku ya kuidhinishwa na Baraza na kuelezwu kwa wafanyakazi wa Chuo Kikuu.

SEHEMU A

KANUNI ZA MAADILI ZA WAFANYAKAZI

Kanuni Namba 1: Utambulisho wa Katoliki

CUHAS ni Chuo Kikuu cha Kikatoliki; Bila kuathiri dini ya mtu, wakati wanatekeleza kazi zao kama wafanyakazi wa Chuo Kikuu, wafanyakazi wote watatakiwa kutanguliza Dhamira ya MMILIKI na kuheshimu **Maadili ya Kikatoliki** ambayo yanajumuisha lakini bila kikomo, mambo yafuatayo:-

- 8. Kuwaheshimu wamiliki wa taasisi na Kanisa Katoliki kwa ujumla
- 9. Kuheshimu utu wa binadamu kama kiumbe kinachoheshimiwa na Mungu **ambako** kunajuuisha:
 - i. Kuheshimu maisha ya binadamu kulingana na Mafundisho ya Kikatoliki
 - ii. Kuheshimu Uhuru wa kila Mtu
 - iii. Kuheshimu Uhuru wa Dini
- 10. Kuheshimu Uumbaji na Mazingira
- 11. Kupenda na Kusamehe
- 12. Haki na Amani
- 13. Kujali na Huruma
- 14. Ukweli na Uadilifu

Kanuni Namba 2:Kuheshimu Mamlaka

Mfanyakazi wa Chuo Kikuu, wakati wote lazima ajiheshimu na aenende katika namna inayooonesha heshima kwa wafanyakazi wenzake ambao wana vyeo vya juu katika mfumo wa madaraka wa Chuo Kikuu, bila kujali tofauti katika mishahara, umri na jinsia, au sifa nyingine zozote, ili mradi

wakati wote kwamba heshima inatolewa kwa ukubwa wa umri kama mila za Kiafrika/Kitanzania zinavyohitaji.

Kanuni Namba 3:Mavazi, Kitambulisho na vinavyofanana navyo:

2.4 Wafanyakazi wenye Sare

Wafanyakazi wote wa Chuo Kikuu, kwa nafasi zao za kipekee na/au mazingira ya kufanya kazi, wanapewa sare au mavazi ya kujikinga n.k., wanatakiwa kuyavaa wakati wa kazi/saa za kazi. Vilevile, mavazi lazima yawe safi, nadhifu na kutunzwa vizuri.

2.5 Wafanyakazi wasio na Sare.

Wafanyakazi wote wa Chuo Kikuu lazima wavae vizuri nguo safi, nadhifu, zenye staha, za kupendeza na zilizotunzwa vizuri (usafi binafsi), kulingana na taratibu za ofisi zinazokubalika.

2.6 Wafanyakazi wote wa Chuo Kikuu lazima wavae **Vitambulisho vinavyoonekana wazi wakati wa saa za kazi na kila wanapokuwa ndani ya maeneo ya taasisi.**

Kanuni namba 4: Lugha / Mawasiliano:

3.3 Wafanyakazi wasiofundisha

Lugha zitakazotumika ni Kiswahili na Kiingereza tu. Lugha nyingine, lahaja na lugha za ishara hazitatumika katika mawasiliano rasmi. Mazungumzo yatafanyika kwa sauti za chini. Hairuhusiwi kutumia lugha ya msimu/kundi maalumu, ya unyanyasaji/isiyo ya heshima.

3.4 Wafanyakazi wanaofundisha

Lugha ya Kiingereza ni lugha rasmi ya kufundishia katika Chuo Kikuu.

Kanuni Namba 5:Utaalamu:

Chuo Kikuu kinaunga mkono maadili ya msingi yafuatayo, ambayo lazima yafuatwe na Wafanyakazi wakati wanapotekeleza majukumu yao:

- (1) *Usawa na Haki*
- (2) *Viwango vya Utaalamu, Taratibu za Maadili*
- (3) *Umahiri wa Taaluma*
- (4) *Uhuru wa Taaluma*
- (5) *Ubunifu*

(6) *Kuheshimu na Kutii Sheria na Katiba ya Nchi*

(7) *Kuendeleza Utambulisho wa Kikatoliki*

5.3 Mwenendo binafasi na wa kitaalamu wa Mfanyakazi unatarajiwa kuthibitisha viwango vya juu vinavyotarajiwa kwa watu katika vyeo vyao. Katika kutekeleza kwa uwezo wa hali ya juu, wafanyakazi wa CUHAS katika majukumu yao watatoa huduma zenye ubora wa hali ya juu kulingana na dhamira ya CUHAS. Katika kufanya hivyo:-

- vi. Wataahidi na kufuata viwango vya utaalamu katika eneo lao la kazi na katika kuchangamana na wateja au wafanyakazi wengine wa Chuo Kikuu
 - vii. Wataahidi kudumisha viwango vya hali ya juu vya uadilifu na ukweli katika kazi yao kwa kufuata viwango vya kimaadili na kisheria
 - viii. Watafuata Kanuni na Maadili ya utaalamu wao unaohusika; na kuwa mfano wa kuigwa na wale walio chini ya usimamizi wao
 - ix. Kutumia kanuni za jamii kulingana na sifa au utaalamu katika utekelezaji wa kazi za mtu na uhusiano na wadau
 - x. Kuwashemtu wafanyakazi wenzake na haki zao ikijumuisha haki ya faragha hasa anaposhughulikia taarifa nyeti na za binafsi.
- 5.4 Wafanyakazi wanawajibika kwa chuo kikuu kuwa na sifa zote (ikijumuisha kudahiliwa na mamlaka sahihi na vyeti vya mazoezi kila mwaka pale inapofaa) ambazo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zao kisheria na kiutaalamu.

Kanuni Namba 6:Matumizi ya Rasilimali, Huduma na Kuepuka Madeni:

- 6.5 Wafanyakazi wote wanawajibika kwa Chuo Kikuu kutotumia, wala kuruhusu matumiai ya mali za Chuo Kikuu, rasilimali au fedha kwa madhumuni tofauti na yaliyoidhinishwa.
- 6.6 Wafanyakazi lazima wapunguze matumizi ya Kompyuta na Kutumia Intaneti kwa madhumuni yanayohusiana na kazi. Wafanyakazi wasitumie muda wa kazi kuingia katika Mitando ya Kijamii, Blogu binafsi au Tovuti za Biashara Mtandaoni. Waajiri wanaweza kufuutilia ufunguaji wa tovuti zisizofaa na kukemea matumizi mabaya ya teknolojia na huduma nyingine. Pia, wafanyakazi wapunguze simu zitumike kwa madhumuni ya kazi.
- 6.7 Wafanyakazi wa Chuo Kikuu hawana mamlaka ya kuingia deni lolote kwa ajili na kwa niaba ya Chuo Kikuu bila ya ridhaa yoyote ya maandishi ya Bodi ya Wadhamini.

-
- 6.8 Wafanyakazi wa Chuo Kikuu wanatakiwa au wanatarajiwa kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika kusimamia mapato yao ili kuepuka kupata matatizo ya kifedha.

Kanuni Namba 7:Kuwapo na/au Kutokuwapo mahali pa kazi

Wafanyakazi wanawajibika kwa Chuo Kikuu kuwapo kazini kama inavyotakiwa na kutokuwapo mahali pa kazi kwa idhini ya MAANDISHI inayofaa na sababu za msingi.

Wafanyakazi wanawajibika kwa Chuo Kikuu kufanya kazi zao katika namna yenyе ufanisi, inayofaa na kwa uhodari, na kuendeleza viwango vya utendaji viliviyotajwa pamoja na kufuata kihalali na kimatiki sera, taratibu, sheria, maelekezo, amri au mwongozo wa mwajiri n.k. na kufanya kazi kama inavyoelekezwa.

7.3 Wakati wa saa za kazi kama unaondoka mahali pa kazi kwa sababu nyingine yoyote tofauti na kwenda uwani:

- 7.3.1 Maofisa wenye Makatibu Muhtasi au Wasimamizi wataacha ujumbe kwa Makatibu Muhtasi wao kuhusu mahali wanapokwenda na muda wanaotarajia kurudi. Wafanyakazi wengine wote watawataarifu wasimamizi wao na kama hawapo watawataarifu Makatibu Muhtasi wa Shule, Taasisi, Kurugenzi au Idara.

7.4 Katika tukio ambapo mfanyakazi hafiki kazini kwa sababu yoyote ile:

- 7.4.1 Wafanyakazi wengine wote wataweza kupata na kutumia njia zozote ndani ya uwezo wao kueleza kwa wasimamizi wao, taarifa kuhusiana na kutokuwapo kwao na sababu za kutofika.

- 7.4.2 Mfanyakazi yejote wa Chuo Kikuu anaweza kuitwa kuja kazini wakati wowote. Kwa hiyo, mfanyakazi yoyote wa Chuo Kikuu anayekusudia kusafiri mbali na mahali alipoajiriwa [kituo cha kazi], atamtaarifu msimamizi wake mapema kuhusu safari hiyo bila kujali kama safari hiyo itafanyika nje ya saa za kazi au siku zisizo za kazi (mwisho wa wiki/sikukuu).

Kanuni Namba 8:Kukubali Zawadi/Manufaa na Tuzo:

- 8.5 Mfanyakazi yejote wa Chuo Kikuu hatashawishi, kuomba, kudai au kukubali ada yoyote, zawadi, bahashishi, kamisheni, faida au tuzo kutoka

kwa ama mfanyakazi mwenzake, marafiki, wanafunzi au umma kwa huduma zilizotolewa au zitakazotolewa au zinazopangwa kutolewa.

- 8.6 Mfanyakazi yeote wa Chuo Kikuu hatapokea zawadi yoyote ya fedha au tuzo au upendeleo kutoka chanzo chochote ambacho kinaweza kuonekana kushawishi uhusiano wa kikazi na hata kama imetolewa bila kushawishi au vinginevyo, lazima ikataliwe.
- 8.7 Kama kanuni ya jumla, zawadi zinazokadiriwa kuwa na thamani ndogo zinakubaliwa. Ambapo thamani ya zawadi inayokadiriwa kuwa zaidi ya TZS. 50,000/= zawadi hiyo **INAPASWA** kukataliwa. **Zawadi ndogo zifuatazo** (zenye thamani ya chini ya TZS 50,000/=) haziko katika kundi la zawadi zinazokataliwa;
- iv. Vitu vyenye thamani ndogo sana ambavyo vimekusudiwa pekee kwa ajili ya uwasilishaji kama vile kadi za salamu, tuzo za ushindi, kalenda, shajara, kalamu, fulana na nyingine kama hizo
 - v. Chochote ambacho mfanyakazi wa CUHAS analipa ua kurejesha thamani yake, na
 - vi. Chochote kinacholipwa na Chuo Kikuu
- 8.8 Zawadi/tuzo za vitu vyenye thamani yoyote (zaidi ya TZS 50,000/= au Inayolingana) tofauti na thamani ya zawadi/ndogo, itaelezwa kwa Makamu Mkuu wa Chuo kutegemeana na thamani yake. Chuo Kikuu, kwa uamuzi wake wa wazi, kitaamua kama kimruhusu mpokeaji kuchukua zawadi au kuelekeza namna ya kuondoa zawadi/tuzo hiyo.

Kanuni Namba 9: Biashara kwa Maslahi Binafsi/Mgongano wa Maslahi:

- 9.8 Kila mfanyakazi wa Chuo Kikuu anatarajiwa kuepuka mazingira ambapo maslahi yake ya kifedha au maslahi mengine binafsi au biashara yanagongana, au yanaweza kuwa na mgongano na maslahi ya Chuo Kikuu. Vivyo hivyo, Chuo Kikuu kinatarajia wafanyakazi wake kutenda kwa maslahi yake wakati wote.
- 9.9 Wafanyakazi HAWATAJIHUSISHA katika shughuli nyingine yoyote, biashara au shughuli ya uwekezaji ambayo inaweza kuingiliana na uwezo wao wa kufanya shughuli zao katika Chuo Kikuu. Pia, wafanyakazi wa Chuo Kikuu WASIJIHUSISHE katika shughuli nyingine yoyote (ya kiutamaduni, kisiasa, burudani, kijamii, kielimu) ambazo zinaweza kugongana na maslahi ya Chuo Kikuu na kuingilia utendaji wa kazi zao.

-
- 9.10 Wafanyakazi wa Chuo Kikuu wasitumie mali yoyote ya Chuo Kikuu, taarifa, cheo au fursa zinazotokana na hayo kwa manufaa binafsi au kushindana au kuharibu sifa ya Chuo Kikuu. Wafanyakazi HAWATAJIHUSISHA katika shughuli YOYOTE, ambayo inaweza kuwa na madhara au kuwa katika ushindani na shughuli za msingi za Chuo Kikuu. Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, “mali za Chuo Kikuu” maana yake ni kitu chochote (kinachoonekana au kisichoonekana) ambacho kilipatikana kwa kutumia jina la Chuo Kikuu.
 - 9.11 Wafanyakazi wa Chuo Kikuu wenyе maslahi ya moja kwa moja au vinginevyo katika kampuni/biashara ambayo inapendekezwa kuhusishwa kutoa huduma kwa Chuo Kikuu wanatakiwa kumtaarifu Makamu Mkuu wa Chuo kuhusiana na hilo, baada ya hapo menejimenti itaamua kama iendelee au isiendelee na uhusishwaji uliopendekezwa. Kushindwa kwa mfanyakazi yejote kuifahamisha menejimenti kuhusu (mfanyakazi) wao kujihusisha katika kampuni/biashara yoyote inayopendekezwa kupewa kazi na Chuo Kikuu, utakuwa ni ukiukaji mkubwa wa kanuni za maadili.
 - 9.12 Hakuna mfanyakazi atakayejihusisha au kupendekeza kujihusisha au kupendekeza uhusishwaji au kushiriki katika shughuli ya kampuni yoyote au biashara ambapo mfanyakazi ana maslahi binafsi kabla ya kutaja au bila ya kutamka maslahi hayo.
 - 9.13 Chuo Kikuu hakitanunua bidhaa ya kampuni/kutoka katika kampuni yoyote ambayo mfanyakazi wa Chuo Kikuu au wanafamilia wake/ndugu wa karibu wana maslahi isipokuwa kama ununuzi huo ni kuitia “zabuni ya umma ya wazi” na tathmini kamili ya mazingira inaonyesha Chuo Kikuu hakitapata matatizo ya aina yoyote, kwa sababu ya ununuzi huo kutoka upande ambao mfanyakazi ana maslahi binafsi.
 - 9.14 Endapo katika mukutano wowote au majadiliano katika shughuli ya Chuo Kikuu, mfanyakazi anayeshiriki katika mukutano/majadiliano ana maslahi binafsi katika jambo linalojadiliwa, atatangaza maslahi yake, ambapo wale wanaoshiriki katika mukutano wataamua kama anaweza kushiriki au kutoshiriki katika kufanya uamuzi kuitia kura ya wazi ya idadi ya waliopo. Mfanyakazi anayehusika atataarifiwa kuhusu uamuzi na sababu za uamuzi huo.

Kanuni Namba 10: Faragha na Siri

Kutokana na ajira katika Chuo Kikuu, Wafanyakazi wanaweza kukabidhiwa taarifa za siri; kuhusiana na Chuo Kikuu na/au washirika wake, wanafunzi wake na wadau wengine. Hata hivyo;

-
- 10.4 Makamu Mkuu wa Chuo ni msemaji pekee wa Chuo Kikuu au ofisa mwingine yeote atakayemuidhinisha ipasavyo kufanya kazi hiyo na kwa maandishi.
- 10.5 Taarifa zote au zozote ambazo mfanyakazi yeote anazipata kutokana na ajira yake ni mali ya Chuo Kikuu. Taarifa hizo hazitatolewa kwa watu wengine bila ya idhini ya maandishi ya Makamu Mkuu wa Chuo, isipokuwa kama taarifa hizo zinatolewa katika utaratibu wa kawaida wa kufanya shughuli za Chuo Kikuu.
- 10.6 Wafanyakazi wote lazima waheshimu faragha za wafanyakazi na wanafunzi na kutumia taarifa zozote za siri kwa madhumuni tu ambayo yalikusudiwa. Kwa hiyo, wafanyakazi HAWATAELEZA kwa watu wasioidhinishwa, taarifa za kiofisi, za siri au vinginevyo, ambazo wameelezwa kwa siri kutoka kwa wengine bila ya idhini na, kutokana na hilo, watatakiwa kutunza siri za taarifa za kiofisi hata baada ya ya kuacha kazi.

Kanuni Namba 11: Utii wa wafanyakazi (Kujituma) kwa Chuo Kikuu na Tabia/Maadili,

- 11.3 Uadilifu wa jumla wa wafanyakazi kwa Chuo Kikuu ni muhimu. Wafanyakazi wote, wakati wote lazima waenende katika namna ya kuunga mkono na kuendeleza sifa nzuri ya Chuo Kikuu, watu wake, dira/dhamira yake na msimamo wake.
- 11.4 Wafanyakazi wataenenda katika namna ambayo hata wakati wanapokuwa nje ya ofisi, tabia zao haziiletei CUHAS sifa mbaya. Hizi zinajumuisha:-
- vii. Matumizi mabaya ya dawa (dawa au pombe),
 - viii. Kucheza kamari
 - ix. Kukopa kiasi kikubwa cha kushindwa kulipa (matatizo ya kifedha),
 - x. Tabia ya vurugu na kujihusisha na masuala ya jamii yanayotia shaka
 - xi. Wafanyakazi waandamizi na walio juu yao (Watendaji wakuu) kukopa kwa wafanyakazi walio chini yao
 - xii. Kukopa kutoka Chuo Kikuu kiasi kinachozidi kiwango kinachoruhusiwa.

Kanuni Namba 12: Udanganyifu

Udanganyifu au kitendo au nia ya udanganyifu, ujanja, kuiba, kulaghai au uongo — yote ni kukosa uaminifu na, mara nyingi, uhalifu.

- 12.3 Wafanyakazi wa Chuo Kikuu wataepuka aina yoyote ya udanganyifu ikijumuisha wizi wa maandishi, kughushi taarifa, data/maandiko, wizi wa hakimiliki na unaofanana na huo. Kwa hali hiyo wizi wa maandishi unajumuisha kazi iliyonakiliwa bila ya kumtambua mwenye kazi, kutoa nakala ya maandiko au kazi usiyoimiliki sehemu yake au yote, njama katika utafiti au chapisho.
- 12.4 Vitendo vya makusudi vya udanganyifu vitachukuliwa hatua kali za kinidhamu, ikijumuisha kufukuzwa kazi ikiwezekana hatua za madai na/au jinai dhidi ya Mfanyakazi anayehusika. **Baadhi ya mifano ya udanganyifu inajumuisha:**
- xiii. Kuwasilisha ripoti zisizo sahihi;
 - xiv. Kughushi au kubuni data;
 - xv. Kujidai ni maofisa wa Chuo kikuu ili kuwadanganya wengine
 - xvi. Kutumia kazi za wengine (zilizoibwa au vinginevyo) kama kazi yako
 - xvii. Kughushi au kubadilisha hundi, matokeo ya mitihani, vyeti n.k.
 - xviii. Kufuja rasilimali au kutumia vibaya mali za Chuo Kikuu;
 - xix. Kushughulikia bila idhini au kuripoti shughuli;
 - xx. Kuongezea idadi ya mauzo;
 - xxi. Kununua bidhaa kwa makusudi zinazojulikana kuwa na kasoro au kinyume na makubaliano;
 - xxii. Kufanya maingizo yoyote katika kumbukumbu za Chuo Kikuu au taarifa za fedha ambazo sio sahihi na kulingana na viwango vizuri vya utunzaji hesabu;
 - xxiii. Kuingia katika makubaliano yasiyoidhinishwa ya kuuza Mali za Chuo Kikuu;
 - xxiv. Udanganyifu kwa kutumia Chuo Kikuu kuingia katika mikataba kwa manufaa binafsi.

Kanuni Namba 13: Matumizi Mabaya ya Pome na Dawa

- 13.3 Kutumia au kuwa na kilevi, dawa haramu na dawa nyingine zinazodhibitiwa mahali pa kazi na kuwa umetumia dawa hizo kazini na

wakati wa saa za kazi kunakatazwa KABISA. Hata hivyo, kuwa na dawa zilizoelekezwa kwa ajili ya matibabu inaruhusiwa.

- 13.4 Kunaweza kuwa na matukio yanayodhaminiwa na Chuo Kikuu ambapo menejimenti imeidhinisha utoaji wa vinywaji vyenye kilevi. Katika matukio hayo, sheria zote za pombe zinazohusika lazima zifuatwe, ikijumuisha sheria kuhusiana na katazo la kutoa pombe kwa wale walio chini ya umri usioruhusiwa kisheria. Hata hivyo, katika matukio yote kama hayo, kunywa kupita kiasi, kulewa na utovu wa nidhamu katika matukio hayo kunakatazwa na kutashughulikiwa vikali.

Kanuni Namba 14: Afya na Usalama

- 14.4 Wafanyakazi wote watafuata kanuni za afya na usalama za Chuo Kikuu kama zinavyoelezwa kwao katika vipindi mbalimbali.
- 14.5 Wafanyakazi wataieleza menejimenti hatari zozote za usalama na afya mahali pa kazi ambazo zinahitaji hatua za masuluhihi.
- 14.6 Wafanyakazi wanahamasishwa kufanya uchunguzi wa afya mara moja kwa mwaka wakati wa kumbukumbu ya siku zao za kuzaliwa.

Kanuni Namba 15: Uhusiano wa Kimapenzi:

- 15.6 Uhusiano wa kimapenzi/kingono baina ya wafanyakazi na wanafunzi unakatazwa kabisa (ndani na nje ya kampasi).
- 15.7 Uhusiano unaochochaea ngono, maneno, kujirahisisha au uhusiano wa karibu wa aina yoyote mahali pa kazi unakatazwa.
- 15.8 Vivyo hivyo, uhusiano kama huo nje ya mahali pa kazi mionganoni mwa wafanyakazi ambao unaingilia kazi ya wafanyakazi unakatazwa kabisa.
- 15.9 Wafanyakazi ambao wako katika uhusiano usio rasmi wanahamasishwa kurasimisha uhusiano huo.
- 15.10 Wenzi wanaofanya kazi pamoja wahakikishe kwamba wanapunguza kuonyesha hisia zao na kushughulikia masuala ya familia, nje ya mahali pa kazi. Uhusiano usiingilie kazi za watumishi. Vilevile, wafanyakazi wenye wenzi ambao sio wafanyakazi wa Chuo Kikuu wasitende katika namna ambayo itaingilia kazi zao (ndani au nje ya kampasi).

Kanuni Namba 16: Unyanyasaji

Chuo Kikuu kinaahidi kutoa mazingira ya kazi ambayo hayana tabia zisizofaa za aina zote za unyanyasaji kwa kuzingatia umri, ulemavu wa mwili, hadhi ya ndoa, rangi, dini, tabaka, jinsi au jinsia. Wafanyakazi wanawajibika kukiunga mkono Chuo Kikuu katika jitihada zake za kuwalinda wengine kutokana na aina yoyote ya unyanyasaji.

- 16.4 Chuo Kikuu hakivumilii unyanyasaji wa Kimwili, Kisaikolojia, kimaneno na Unyanyasaji wa Kingono. Kwa hiyo, wafanyakazi HAWATAJIHUSISHA katika tabia kama hiyo wakati wowote, iwe mahali pa kazi au nje ya mahali pa kazi wakati wakiwa katika ajira ya Chuo Kikuu.
- 16.5 Kila unyanyasaji unapotokea kwa mfanyakazi yejote kutokana na kutenda au kutotenda kwa mtu mwingine yejote au mgeni, wakati wa mfanyakazi kutekeleza kazi zake; Chuo Kikuu kitachukua hatua zote muhimu na zinazofaa kusaidia wafanyakazi walioathirika kuhusiana na hatua za kusaidia na kuzuia.
- 16.6 Unyanyasaji wa aina yoyote hautavumiliwa. Masuala yote yanayohusiana na unyanyasaji wa kingono hayatavumiliwa. Masuala yote yanayohusiana na unyanyasaji wa kingono yatashughulikiwa kulingana na masharti ya Sera za Unyanyasaji wa Jinsia na Unyanyasaji wa Kingono.

Kanuni Namba 17: Kufuata Sheria

- 17.3 Wafanyakazi wote watafanya kazi zao kulingana na sheria na kanuni zote zinazohusika za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- 17.4 Wafanyakazi wa CUHAS watajielimisha wenyewe kwa sheria, kanuni na taratibu zilizopo na kuzifuata ipasavyo.

SEHEMU B

18.0 MATUMIZI, UDHIBITI NA UTOAJI WA ADHABU ZA KINIDHAMU KWA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAADILI

18.3 Sera na Taratibu Rasmi za Kinidhamu

Uzoefu wa Chuo Kikuu umeshuhudia kwamba wafanyakazi walio wengi wanafanya kazi vizuri, wana tabia nzuri na kukabiliana na matatizo madogo bila ya kuhitaji hatua rasmi za kinidhamu. Kimsingi matatizo yanashughulikiwa (mf. Ushauri/Unasihi) kwa matarajio kwamba wafanyakazi watajitatihidi kadri ya uwezo wao mara tu upungufu utakapoonyeshwa na kwamba matatizo yoyote yanaweza kukabiliwa katika ngazi ya mahali pa kazi. Pale ambapo Chuo Kikuu kina sababu ya kuamini kwamba kiwango kizuri cha utendaji hakikufikiwa na kudumishwa au kwamba Kanuni za Maadili vinginevyo zimekiukwa, taratibu rasmi za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mfanyakazi huyo.

18.4 Kukiuka Kanuni za Maadili

- 18.4.1 Kukiuka Kanuni za Maadili inamaanisha mwenendo wowote mbaya, kitendo au kutenda au kutotenda kunakofanywa na mfanyakazi katika ukiukaji wa wajibu kama ilivyoelezwa hapo juu na kwa mujibu wa mkataba wa ajira. Kama itajulikana, mwenendo mbaya unaweza kusababisha kupewa onyo au karipio. Kurudia kosa au utovu mkubwa wa nidhamu, kama ukigundulika, utasababisha kusimamishwa kazi au kufutwa kazi papo hapo.
- 18.4.2 Kwa kuzingatia malengo ya Kanuni za Maadili za Wafanyakazi wa Chuo Kikuu, ukiukaji wowote utasababisha kutumika kwa adhabu zinazofaa kama ilivyoelezwa katika Kanuni za Utumishi na katika Kanuni hizi.
- 18.4.3 Utovu wa nidhamu au kujirudia kwa utovu wa nidhamu ni tabia ambayo inadhoofisha uhusiano wa kimkataba wa ajira kati ya mfanyakazi na mwajiri. Hali hiyo inaatishia ustawi wa Chuo Kikuu kama taasisi au wafanyakazi au wanafunzi au mgeni. Mifano ya utovu wa nidhamu inajumuisha ifuatayo, lakini bila kikomo: -
- ix. Kushindwa kufanya vizuri kazi zilizoainishwa au kutofuata maelekezo ambayo ni halali na ya kuridhisha yanayotolewa na wasimamizi.

-
- x. Kumshambulia au kutishia kumshambulia msimamizi wako, mfanyakazi mwenzako, mwanafunzi au mgeni katika maeneo ya Chuo Kikuu.
 - xi. Kutenda katika namna inayosababisha hatari ya usalama kwa wafanyakazi, wanafunzi au mali kama vile kuvuta sigara katika maeneo yaliyotengwa kama yenye hatari au yanayokatazwa au matumizi yasiyoruhusiwa ya uzuiaji wa moto au vifaa vya usalama au vifaa vinavyofanana na hivyo.
 - xii. Kuathiriwa na pombe au dawa “zisizoagizwa na daktari” unapokuwa kazini au katika maeneo ya Chuo Kikuu.
 - xiii. Kumiliki bila idhini, au kuondoa mali inayomilikiwa na Chuo Kikuu, mfanyakazi mwingine, mwanafunzi au mgeni wa Chuo Kikuu.
 - xiv. Kuwasilisha madai ya uongo kwa kukusudia kuhusu jambo lolote kwa ajili ya kulipwa au vinginevyo na/au udanganyifu mwingine wowote wa kumbukumbu au nyaraka za Chuo Kikuu.
 - xv. Kutenda kwa makusudi au kwa uzembe au kushindwa kutenda katika namna ya kuwajibika kunakosababisha madhara kwa mali ya Chuo Kikuu au mfanyakazi au mwanafunzi au mgeni.
 - xvi. Kurudia kukiuka Kanuni za Maadili.

Ukiukaji wote au wowote kati ya uliyotajwa hapo juu na unaofanana nao utasababisha kupewa adhabu kwa mujibu wa kanuni za nidhamu kwa njia ya onyo la mdomo na/au maandishi, faini, karipio, karipio kali, kusimamishwa kazi na/au kufukuzwa papo hapo kulingana na matumizi ya Sheria ya Ajira.

SEHEMU C

18.0 HAKI ZA WAFANYAKAZI NA WAJIBU WA WAFANYAKAZI ENDAPO HATUA YA KINIDHAMU ITACHUKULIWA

18.3 Chuo Kikuu kufuata taratibu za kisheria katika kuchukua hatua za kinidhamu.

Haki za wafanyakazi wa Chuo Kikuu kuhusiana na hatua ya kinidhamu zimeelezwa katika sheria ya ajira, ambayo inaanadaa kanuni zinazounda taratibu za haki kwa hatua za kinidhamu mahali pa kazi. Chuo Kikuu kitafuata taratibu hizo. Kwa mfano, kanuni ya kufanya uamuzi wa haki ambayo inaeleza:-

- Mfanyakazi lazima apate taarifa ya maandishi ya tuhuma mahususi ya utovu wa nidhamu na apewe muda wa kutosha kujibu kwa maandishi (muda usiopungua siku14).
- Lazima kuwe na fursa kwa mfanyakazi mwenyewe kuwepo ili kueleza au kukanusha tuhuma mbele ya Mamlaka ya Ajira/Nidhamu/Kamati ya Chuo Kikuu.
- Mamlaka ya Ajira/Nidhamu lazima ichukue hatua ipasavyo na kuhakikisha hakuna upendeleo katika maelezo ya mfanyakazi ya maandishi na ya mdomo kabla ya kuamua.
- Adhabu za kinidhamu zitakazotolewa lazima ziwe za kisheria.

18.4 ADHABU ZA KINIDHAMU

18.4.1 Onyo

18.4.1.1 Mfanyakazi yejote anastahili kuonywa kuhusiana na kukiuka kanuni ya nidhamu na kuelezwaa namna ambavyo utendaji au tabia lazima iboreshwe. Maonyo yanaweza kutolewa kwa mdomo na/au kwa maandishi. Chuo Kikuu kitathibitisha maonyo rasmi kwa maandishi kwa ajili ya kumbukumbu na kwa mujibu wa kanuni ya nidhamu.

Onyo rasmi litajumuisha lakini bila kikomo mambo yafuatayo:-

- Maelezo ya tatizo.
- Kanuni/kiwango au sera ya Chuo Kikuu iliyokiukwa.
- Hatua ya marekebisho inayotakiwa.
- Kipindi ambacho hatua ya marekebisho lazima ichukuliwe.

-
- Kumbukumbu ya mikutano na mfanyakazi na maelezo yoyote aliyojatoa.
 - Uamuzi wa Mamlaka ya Ajira/Nidhamu ya Chuo Kikuu.
 - Madhara ya kushindwa kuchukua hatua za marekebisho au ukiukaji mwingine zaidi.
 - Kumbukumbu ya maonyo yoyote yaliyotangulia; kama yapo ya nyuma.

18.4.2 Kusimamishwa Kazi.

Pale ambapo ukiukaji wa kinidhamu umetokea, Chuo Kikuu kinaweza kumwelekeza mfanyakazi kutoendelea kuwapo mahali pa kazi (kusimamishwa). Hii ni kuruhusu jambo hili linalohusika kuchunguzwa kwa kina. Kanuni na masharti ya kusimamishwa yataongozwa na sheria ya ajira.

18.4.3 Kufukuzwa kazi kwa Sababu za kinidhamu

Ukiukaji wowote wa kanuni ya maadili unaosababisha kufukuzwa kazi, adhabu hiyo itatolewa kulingana na taratibu za ajira ya wafanyakazi/nidhamu za Chuo Kikuu kulingana na masharti ya Sheria ya ajira.

SEHEMU D:

19.0 MAKOSA YANAYOFANYWA NA MFANYAKAZI TOFAUTI NA YALE YA KINIDHAMU

- 19.3 Mfanyakazi yeote wa Chuo Kikuu anayefanya kosa la jinai atashughulikiwa na Jamhuri.
- 19.4 Mfanyakazi wa Chuo Kikuu ambaye amefanya kosa la jinai [mf. wizi] mahali pa kazi, atasimamishwa kazi mara moja au hatua za kinidhamu zinazofaa zitachukuliwa; na baada ya hapo atashtakiwa mahakamani.

Agosti 2018